WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Baraza la Kiswahili la Taifa
BAKITA

UNESCO

# IKISIRI ZA

## KONGAMANO LA PILI LA KISWAHILI LA KIMATAIFA

**PARIS, UFARANSA | 4-7 Julai 2026**

**“Kiswahili kwa Amani, Mshikamano na Diplomasia ya Uchumi Duniani”**



WIZARA YA HABARI,
UTAMADUNI, SANAA
NA MICHEZO

# IKISIRI ZA

## KONGAMANO LA PILI LA KISWAHILI LA KIMATAIFA

**PARIS, UFARANSA**

**Tarehe 4-7 Julai 2026**

**"Kiswahili kwa Amani, Mshikamano na Diplomasia ya Uchumi Duniani"**

© WHUSM, CHALUFAKITA & CHAUKIDU - 2026

# Yaliyomo

**Yaliyomo ........................................................................ iii**
**Utangulizi.......................................................................... vii**
**Jedwali la Wawasilishaji ..........................................................1**
**Tafsiri kama Diplomasia ya Kitamaduni:**
**Abdulrazak Gurnah na Utambulisho wa Kiswahili .............6**
*Ida Hadjivayanis ........................................................................ 6*
**Kiswahili na Vijana..................................................................7**
*Zawadi Sakapalla........................................................................ 7*
**Mchango wa Riwaya ya Kiswahili katika Kufundisha**
**Diplomasia: Mfano wa Riwaya ya *Kusadikika* .......................8**
*Athumani S. Ponera ................................................................... 8*
**Ukiona Vyaelea Vimeundwa: Mchango wa Tanzania**
**katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani................................9**
*Mussa. M. Hans ......................................................................... 9*
**Ufanisi wa Kiswahili katika Kujenga Umoja na**
**Maendeleo Madhubuti ya Afrika Kupitia Teknolojia**
**ya Akili Unde (AU)..................................................................11**
*Aldin Mutembei ........................................................................ 11*
**Mdhihiriko wa Mitindo ya Lugha katika Hotuba za**
**Rais Dkt. Mwinyi katika Kuhimiza Amani,**
**Mshikamano na Maendeleo .................................................13**
*Riziki Pembe Juma & Ahmad Yahya Sovu.............................. 13*
**Nafasi ya Nyimbo za Kiswahili katika Kujenga**
**Utangamano wa Kimataifa: Mfano wa Nyimbo Teule**
**za Diamond Platinumz ..........................................................14**

*Adria Fuluge & Davian Buguna* ............................................ *14*
**Kiswahili katika Ustawi wa Vijana na Nafasi Yake katika Kudumisha Amani na Maendeleo Endelevu kwa Vijana Afrika Mashariki** .............................................**15**
*Ali Haji Hassan* ........................................................................ *15*
**Ubunifu wa Kaulimbiu za Kiswahili za Kuhamasisha Amani Nchini Tanzania** .......................................................**16**
*Alpha Kavishe, Issaya Lupogo & Mustapha Almasi* .............. *16*
**Tafsiri katika Kiswahili na Mabadiliko ya Uchumi wa Kidijiti** ...........................................................................**17**
*Amour Salim Said* ..................................................................... *17*
**Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza Uchumi wa Taifa la Tanzania** ......................................................................**18**
*Anna N. Kyamba* ....................................................................... *18*
**Sera ya lugha nchini Burundi na athari zake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili** ..............................**19**
*Bamporubusa Mathieu* ............................................................. *19*
**Kiswahili na Utangamano wa Kimataifa** ............................**20**
*Chifu Said Mohamed Said (Chifu Kapere)* ............................ *20*
*mwenekapufi@gmail.com* ......................................................... *20*
**Onomastiki ya Ulemavu katika Methali za Waswahili: Elimu kwa Mtazamo wa Maarifa Asili** ...........**21**
*Wanjala C. N. Simiyu* ................................................................ *21*
*wsimiyu@kibu.ac.ke* .................................................................. *21*
**Mbinu za Uhunthishaji wa Wahusika katika Filamu za Kiswahili: Mifano kutoka Vichekesho vya Joti na Dulvani** ...........................................................................**23**
*Diana Remias* ............................................................................. *23*

**Kiswahili na Amani.........................................................................24**
*Elizabeth Luena Lyimma.......................................................... 24*
**Matumizi ya Akiliunde kama Nyenzo ya Tafsiri katika Ujifunzaji wa Kiswahili: Uzoefu Kutoka Chuo Kikuu cha Ghana ..................................................................25**
*Hadija Jilala ............................................................................ 25*
**Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza Uchumi Baina Tanzania na Comoro ..........................................................26**
**Nguvu ya Kiswahili katika Diplomasia ya Kiutamaduni na Maendeleo ya Utalii ..................................27**
*Lorna B. Mwijarubi ................................................................. 27*
**Dhima ya Lugha katika Kuibua Wanadiplomasia Bobevu: Uchunguzi katika Ufundishaji Kiswahili katika Ngazi ya Elimumsingi ..............................................28**
*Maryam Y. Mwinyi.................................................................. 28*
**Nafasi ya Kiswahili katika Utangamano wa Kimataifa kwa jicho la Ubuntu ............................................29**
*Meinrad Haule Lembuka ......................................................... 29*
*meinradlembuka@gmail.com ................................................ 29*
**Nafasi ya Kiswahili katika Kujenga Utangamano wa Kimataifa nchini Uganda ...................................................30**
*Monday Geofrey Akol Amazima ............................................. 30*
*mwalimakol@gmail.com.......................................................... 30*
**Dhima ya Kiswahili katika Kujenga Utambulisho wa Kitaifa kupitia Mfumo wa Elimu ........................................31**
*Saade Said Mbarouk, Mwanahija Ali Juma na Asha L. Ibrahim.................................................................................. 31*
*mwanahijajuma1@gmail.com ............................................... 31*

**Nafasi ya Akiliunde katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Mkabala wa Kimawasiliano ....................33**
*Nasra Habibu & Salma Hamad* .................... 33
*nasramtani@gmail.com* .................... 33
**Kiswahili: Msingi wa Uhuru wa Kidijiti kwa Vijana ....................35**
*Onesmo S. Nyinondi* .................... 35
**Kusimamia Haki ya Kijamii Darasani: Uchunguzi wa Mbinu za Ukuzaji wa Kiswahili katika Mazingira ya Kielimu Yenye Lugha Nyingi ....................36**
*Said S. Khassim* .................... 36
**Mchango wa Akiliunde katika Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kwenye Diplomasia ya Kidijiti na Uchumi wa Dunia ....................37**
*Shaban Rashid Said* .................... 37
*kisleufahari@gmail.com* .................... 37
**Urazini wa Diplomasia ya Uchumi katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Makuwadi wa Soko Huria* ....................38**
*Stela Faustine* .................... 38
**Uchunguzi wa Matumizi ya Kiswahili katika Huduma za Hoteli kwa Watalii wa Kigeni: Mtazamo wa Watalii kutoka Ufaransa Jijini Arusha ....................39**
*Theresia Bonface Mbogo* .................... 39
**Matumizi ya Fasihi ya Kiswahili katika Diplomasia ya Umma na Maendeleo ya Uchumi Endelevu ....................41**
*Neema Julius Luhwago* .................... 41
**Kwa Nini ni Lazima Kuenzi Utamaduni Wetu? ....................43**

*Omar Salum Mohamed* ........................................................... 43
**Nafasi ya Kiswahili katika Kuhamasisha Diplomasia na Maendeleo ya Uchumi Duniani** .......................................**44**
*Sarah Vincent*................................................................... 44
**Uhifadhi wa Urithi wa Kiswahili kwa Utalii Endelevu: Mfumo wa Kitaifa wa Mikusanyiko ya Kiswahili kupitia Bibliografia ya Taifa**................................**46**
*Mboni A. Ruzegea* ....................................................... 46



# Utangulizi



Kitabu hiki kina ikisiri za makala thelathini na tatu kwa ajili ya kuwasilishwa katika Kongamano la Kimataifa la Kiswahili litakalofanyika Paris, Ufaransa. Ikisiri zote zinaegemea katika mada kuu ya Kongamano hili ambayo ni **Nafasi ya Kiswahili katika Ustawi wa Kidiplomasia na Kiuchumi**. Ikisiri hizo ni za wawasilishaji wanaotoka katika nchi mbalimbali duniani, hivyo kukamilisha dhana ya umataifa wa Kongamano hili.

Makala zinazotarajiwa kuwasilishwa zinaangazia maeneo mbalimbali ya isimu, fasihi, na utamaduni wa Mswahili. Aidha, makala hizo zinaangazia masuala mtambuko yanahusiana na lugha ya Kiswahili. Zaidi, kuna makala zinazothibitisha kuwa Kiswahili kimekwishachuchuka na kuanza kubeba majukumu makubwa ya kuzisemea taaluma nyingine kama vile kilimo, mazingira, afya, ulinzi, siasa, usalama, falsafa, na TEHAMA.

Kila ikisiri ina vipengele vifuatavyo: anwani ya makala, jina la mwasilishaji au wawasilishaji pamoja na anwani ya baruapepe. Vipengele hivi ni muhimu kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji wa maudhui ya makala husika kwa siku za baadaye (kwa kuwasiliana na mwasilishaji) pamoja na kuimarisha 'usemezano wa kitaaluma'.

# Jedwali la Wawasilishaji

| # | Mada ya Makala | Jina la Mwasilishaji na Nchi Anayotoka |
|---|---|---|
| 1. | Tafsiri kama Diplomasia ya Kitamaduni: Abdulrazak Gurnah na Utambulisho wa Kiswahili | Ida Hadjivayanis - Uingereza |
| 2. | Kiswahili na Vijana | Zawadi Sakapalla - Marekani |
| 3. | Mchango wa Riwaya ya Kiswahili katika Kufundisha Diplomasia: Mfano wa Riwaya ya *Kusadikika* | Athumani S. Ponera - Tanzania |
| 4. | Ukiona Vyaelea Vimeundwa: Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani | Mussa. M. Hans - Tanzania |
| 5. | Ufanisi wa Kiswahili katika Kujenga Umoja na Maendeleo Madhubuti ya Afrika Kupitia Teknolojia ya Akili Unde (AU) | Aldin Mutembei - Tanzania |
| 6. | Mdhihiriko wa Mitindo | |

| | | |
|---|---|---|
| | ya Lugha katika Hotuba za Rais Dkt. Mwinyi katika Kuhimiza Amani, Mshikamano na Maendeleo | Riziki Pembe Juma & Ahmad Y. Sovu - Tanzania |
| 7. | Kiswahili na Uchumi | Ibrahima Ibrahim - Comoro |
| 8. | Ubunifu wa Kaulimbiu za Kiswahili za Kuhamasisha Amani Nchini Tanzania | Alpha Kavishe, Issaya Lupogo & Mustapha Almasi - Tanzania |
| 9. | Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza Uchumi wa Taifa la Tanzania | Anna N. Kyamba - Tanzania |
| 10. | Kusimamia Haki ya Kijamii Darasani: Uchunguzi wa Mbinu za Ukuzaji wa Kiswahili katika Mazingira ya Kielimu Yenye Lugha Nyingi | Said S. Khassim - Uholanzi |
| 11. | Sera ya lugha nchini Burundi na athari zake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili | Bamporubusa Mathieu - Burundi |
| 12. | Kiswahili na Diplomasia | Chifu Said Mohamed Said (Chifu Kapere) - Tanzania |
| 13. | Nafasi ya Muziki katika Kujenga Utangamano wa Kimataifa | Adria Fuluge & Davian Buguna - Tanzania |
| 14. | Matumizi ya Akiliunde | |

| | | |
|---|---|---|
| | kama Nyenzo ya Tafsiri katika Ujifunzaji wa Kiswahili: Uzoefu Kutoka Chuo Kikuu cha Ghana | Hadija Jilala - Tanzania |
| 15. | Nguvu ya Kiswahili Katika Diplomasia ya Kitamaduni na Maendeleo ya Utalii | Lorna B. Mwijarubi - Tanzania |
| 16. | Dhima ya Kiswahili katika ElimuMsingi: Chimbuko la Wana Diplomasia Bobevu | Maryam Y. Mwinyi - Tanzania |
| 17. | Mapitio ya Nafasi ya Kiswahili katika Utangamano wa Kimataifa kwa jicho la Ubuntu | Meinrad Haule Lembuka - Tanzania |
| 18. | Tafsiri katika Kiswahili na Mabadiliko ya Uchumi wa Kidijiti | Amour S. Said Zanzibar - Tanzania |
| 19. | Nafasi ya Akiliunde katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Mkabala wa Kimawasiliano | Nasra Habibu na Salma Hamad - Tanzania |
| 20. | Kiswahili: Msingi wa Uhuru wa Kidijitali kwa Vijana | Onesmo S. Nyinondi - Tanzania |
| 21. | Dhima ya Kiswahili katika Kujenga Utambulisho wa Kitaifa Kupitia Mfumo wa Elimu | Saade Said Mbarouk, Mwanahija Ali Juma na Asha L. Ibrahim |

| | | |
|---|---|---|
| | | - Tanzania |
| 22. | Mchango wa Akiliunde katika Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kwenye Diplomasia ya Kidijiti na Uchumi wa Dunia | Shaban Rashid Said - Tanzania |
| 23. | Onomastiki ya Ulemavu katika Methali za Waswahili: Elimu kwa Mtzamo wa Maarifa Asili | Wanjala Simiyu - Kenya |
| 24. | Urazini wa Diplomasia ya Uchumi katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Makuwadi wa Soko Huria* (Chachage, 2002) | Stela Faustine-Tanzania |
| | Nafasi ya Kiswahili katika kujenga utangamano wa kimataifa nchini Uganda | Monday Geofrey Akol Amazima - Uganda |
| 25. | Mbinu za Uhunthishaji wa Wahusika katika Filamu za Kiswahili: Mifano kutoka Vichekesho vya Joti na Dulvani. | Diana Remias - Tanzania |
| 26. | Kiswahili na Amani | Elizabeth Luena Lyimma - Tanzania |
| 27. | Kiswahili katika Ustawi | |

| | | |
|---|---|---|
| | wa Vijana na Nafasi Yake katika Kudumisha Amani na Maendeleo Endelevu kwa Vijana Afrika Mashariki | Ali Haji Hassan - Tanzania |
| 28. | Uchanganuzi wa Kimaeneo wa Matumizi ya Kiswahili katika Huduma za Utalii kwa Wageni Nchini Tanzania | Theresia Bonface Mbogo - Tanzania |
| 29. | Matumizi ya Fasihi ya Kiswahili katika Diplomasia ya Umma na Maendeleo ya Uchumi Endelevu | Neema Julius Luhwago |
| 30. | Nafasi ya Kiswahili katika Kuhamasisha Diplomasia na Maendeleo ya Uchumi Duniani | Sarah Vincent |
| 31. | Kwa Nini ni Lazima Kuenzi Utamaduni Wetu? | Omar Salum Mohamed |
| 32. | Uhifadhi wa Urithi wa Kiswahili kwa Utalii Endelevu: Mfumo wa Kitaifa wa Mikusanyiko ya Kiswahili kupitia Bibliografia ya Taifa | Mboni A. Ruzegea Tanzania |

# Tafsiri kama Diplomasia ya Kitamaduni: Abdulrazak Gurnah na Utambulisho wa Kiswahili



**Ida Hadjivayanis**

ih11@soas.ac.uk

Tafsiri ya fasihi inazidi kuwa chombo muhimu katika diplomasia ya kitamaduni, ikirahisisha usambazaji wa simulizi zinazoendeleza uelewa wa kitamaduni na ule wa uhusiano wa kimataifa. Kwa kutumia tafsiri za kazi za kifasihi za Abdulrazak Gurnah kama kielelezo, wasilisho hili linafafanua jinsi tafsiri inavyofanya kazi ya kuwa kielelezo cha mitazamo ya kidunia na utambulisho wa Waswahili duniani. Kwa kiasi kikubwa, riwaya za Gurnah zilizojikita katika historia binafsi, kumbukumbu za mwambao wa Bahari ya Hindi, na kumbukumbu za ukoloni huchukua maana tofauti zinaposafiri na kuingia katika lugha na tamaduni nyingine. Je, tafsiri hizi huchukua taswira gani zinaporudi katika lugha ya Kiswahili? Tafsiri pekee za Gurnah katika lugha za Kiafrika ni zile zilizofanywa na Hadjivayanis kwa Kiswahili, *Peponi (2022)* na *Dhulma (2025)*. Je, tafsiri hizo zina nafasi gani katika diplomasia ya kitamaduni ya Kiswahili? Inakubalika kwamba zinapotafsiriwa katika lugha za kigeni kama Kifaransa na Kichina, hupanua wigo wa wasomaji na kuengua simulizi finyu kuhusu Afrika. Inakuwaje zinaposafiri katika lugha ya Kiswahili?

## Kiswahili na Vijana



**Zawadi Sakapalla**

SakapallaCC@gmail.com

Lengo la makala hii ni kueleza jinsi Kiswahili kilivyo na nafasi katika kuwajengea vijana hali ya kujitambua, kujiamini, na kuendeleza utamaduni wetu, hasa kwa watoto wanaokulia nje ya Tanzania. Makala inatoa mifano halisi kutoka katika kazi kama vile Let's Go *Volunteer, Twende Tukajitolee* na vitabu vya kuchora. Makala inadhihirisha kuwa, kupitia vitabu hivyo, Kiswahili kinaweza kuimarisha uhusiano wa kifamilia, kijamii, na kitaifa, hasa watoto wa diaspora wanapoweza kuwasiliana na ndugu bila vikwazo. Zaidi, makala inatoa mifano ya jinsi Kiswahili kinavyotumika katika programu za maendeleo ya vijana kupitia hadithi za kiutamaduni, mafunzo ya elimu ya fedha, na programu za kujitolea. Programu hizi huwapa vijana nafasi ya kutumia Kiswahili katika mazingira halisi huku wakijielimisha, kubadilishana utamaduni, na kushiriki katika miradi ya maendeleo ya jamii. Makala pia inaonesha kwa mifano kuhusu vijana wa diaspora ya Kitanzania walioshiriki programu hizi na baadaye kukubaliwa katika vyuo vikuu kama Harvard, Yale, Columbia, na Duke. Mafanikio yao yanaonyesha kuwa misingi ya utamaduni, uongozi, kujitolea, na kujiamini kwa lugha mbili huimarisha ubora wa kitaaluma.

# Mchango wa Riwaya ya Kiswahili katika Kufundisha Diplomasia: Mfano wa Riwaya ya Kusadikika



**Athumani S. Ponera**

atponeraman@gmail.com / athuman.ponera@udom.ac.tz

Makala hii inajadili namna mwandishi wa riwaya ya *Kusadikika* anavyoifunza jamii kuhusu misingi, aina, na umuhimu wa diplomasia katika kuistawisha jamii. Utafiti uliozaa makala hii ulifanyika maktabani, huku ukijiegemeza katika mkabala wa kitaamuli. Ikitumia Nadharia ya Uhemenitiki, makala inabainisha kuwa riwaya ya *Kusadikika* imeakisi aina, misingi, na umuhimu wa diplomasia katika kuendeleza jamii. Kuhusu aina, riwaya imetumia *diplomasia ya kibalozi* kupitia wajumbe sita waliotumwa katika nchi zote zinazopakana na nchi ya Kusadikika. Riwaya inahimiza misingi ifuatayo ya kidiplomasia ili kupata ustawi: Kusadikika ishirikiane na nchi nyingine; yafanyike majadiliano ili kuijenga Kusadikika; kuthamini utu wa wana-Kusadikika wote; Kusadikika iwe na ustawi unaolandana na nchi jirani; kila mwana-Kusadikika awajibike katika kuijenga nchi; na kila mwana-Kusadikika awe mwadilifu. Riwaya inaonesha kuwa diplomasia husaidia: kuushikamanisha ulimwengu; kudumisha amani ulimwenguni; na kulinganishia ustawi wa jamii katika nyanja mbalimbali. Makala inahitimisha kuwa riwaya teule ina maudhui faafu katika kufundisha diplomasia; hivyo haina budi kuendelea kufundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu.

# Ukiona Vyaelea Vimeundwa: Mchango wa Tanzania katika Maendeleo ya Kiswahili Duniani



**Mussa. M. Hans**

hansmussa@udsm.ac.tz/ mussahans30@gmail.com

Ni vigumu sana kutaja maendeleo ya Kiswahili ndani na nje ya Bara la Afrika bila kuitaja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kuanzia sasa, Tanzania). Tanzania ni nchi pekee duniani yenye mabaraza mawili ya Kiswahili. Pia, nchini Tanzania kuna vyuo vikuu viwili (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar) ambapo kila Chuo kina Idara mbili zote zinasimamia utafiti na ufundishaji katika lugha ya Kiswahili. Aidha, nchi ya Tanzania ina sera, mipango, na mikakati mbalimbali inayohusu lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa mikakati hiyo ni mkakati wa kitaifa wa ubidhaishaji wa Lugha ya Kiswahili 2022-2032. Jitihada hizi kitaifa zilianza hata kabla ya kupata uhuru. Mathalani, tarehe 7 Julai 1954 chama cha TANU kilitangaza rasmi Kiswahili kuwa lugha ya ukombozi. Aidha, uamuzi wa kuteua tarehe 7 Julai kuwa Siku ya Kiswahili Duniani mbali na mambo mengine umefanywa kwa kuzingatia usuli huo. Makala hii inalenga kubainisha mchango wa Tanzania katika maendeleo ya Kiswahili. Mbali na mambo mengine, mchango huu utabainishwa kupitia tathmini ya utekelezaji wa mkakati wa taifa wa kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi. Katika tathmini hiyo tutabainisha mafanikio,

changamoto na fursa zilizopo. Data za utafiti uliozaa makala hii zimepatikana kwa kutumia njia mbili ambazo ni upitiaji wa nyaraka za maktabani na usaili.

# Ufanisi wa Kiswahili katika Kujenga Umoja na Maendeleo Madhubuti ya Afrika Kupitia Teknolojia ya Akili Unde (AU)



**Aldin Mutembei**

kaimutembei@gmail.com

Makala hii inafafanua jukumu la kimkakati la Kiswahili kama lugha ya mawasiliano katika kukuza umoja wa Kiafrika na maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika muktadha wa teknolojia za AkiliUnde (AU). Kwa kuzingatia nadharia za lugha na maendeleo, utafiti uliozaa makala hii unasisitiza kwamba kufundisha na kujifunza Kiswahili kupitia lugha nyingine za asili za Afrika kutaongeza ushirikishwaji, uelewekaji na kujiona wamoja; hivyo kuimarisha mshikamano na Umoja wa Afrika. Aidha, makala inajadili kuwa matumizi ya teknolojia ya AU katika elimu ya lugha na lugha ya Kiswahili yanatoa fursa mpya katika ujuzi wa uhifadhi wa lugha za asili, mawasiliano ya kitamaduni, na kuchochea uvumbuzi wa kiteknolojia. Kupitia uchambuzi wa machapisho yanayohusu elimu ya lugha mbalimbali za Afrika, sera za lugha barani Afrika, na teknolojia za AU katika lugha, makala hii inadhihirisha kwamba Kiswahili kinaweza kutumika kama nyenzo ya umoja wa kitamaduni na maendeleo ya kiuchumi na kijamii endapo kitaungwa mkono na suluhisho za AU zinazoheshimu ikolojia ya lugha za asili za Afrika.

**Dhana za msingi**: Teknolojia za AU, nadharia ya lugha na maendeleo, sera, ikolojia.



# Mdhihiriko wa Mitindo ya Lugha katika Hotuba za Rais Dkt. Mwinyi katika Kuhimiza Amani, Mshikamano na Maendeleo



**Riziki Pembe Juma & Ahmad Yahya Sovu**

*rikikijamal@yahoo.com* & *sovu82@gmail.com*

Makala hii inafafanua namna mitindo ya lugha inayodhihirika katika hotuba za Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar, katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2025 na inavyohimiza amani, mshikamano na maendeleo. Data za makala zilikusanywa kwa kutumia mbinu kuu tatu: mahojiano, hojaji, na udurusu wa maktabani. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Ushawishi. Matokeo yamedhihirisha kuwa katika hotuba zake, Mhe. Rais Mwinyi hutumia mitindo ifuatayo ya lugha: takwimu, ucheshi, tafsida, misemo, majazi, tashbiha, takriri, masimulizi ya hadithi na kuchanganya msimbo. Pia, imebainika kuwa mitindo hiyo hutumika kama zana za kutuliza misuguano, kuhimiza maridhiano na kuwaleta wananchi pamoja katika ajenda za maendeleo. Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mitindo katika hotuba za Mhe. Rais Mwinyi si mapambo ya lugha pekee, bali ni mbinu mahsusi za kujenga fikra shirikishi, kuendeleza amani na kuimarisha mshikamano wa kijamii visiwani Zanzibar.

**Maneno Muhimu**: Mitindo, Amani, mshikamano



# Nafasi ya Muziki katika Kujenga Utangamano wa Kimataifa



**Adria Fuluge & Davian Buguna**

adriafuluge@yahoo.com &
davianbuguna@mzumbe.ac.tz

Jamii mbalimbali duniani hutumia utanzu wa nyimbo kwa namna tofauti zinapokabiliana na shughuli zake za kila siku. Makala hii inafafanua nafasi ya nyimbo za Kiswahili katika kujenga utangamano wa kimataifa kwa kurejelea nyimbo teule za Diamond Platinumz. Makala inabainisha jinsi maudhui, matumizi ya lugha ya Kiswahili, pamoja na mitindo ya nyimbo hizo inavyochangia katika kueneza utamaduni wa Kiswahili na kukuza uelewano miongoni mwa jamii za mataifa mbalimbali. Makala inaongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui, data zilikusanywa kutoka katika nyimbo teule na kuchambuliwa. Makala inabainisha kuwa nyimbo za Kiswahili zina nafasi muhimu katika kuvuka mipaka ya kitaifa na kuimarisha mahusiano ya kiutamaduni. Zaidi, inaonesha namna majukwaa ya kidijiti yalivyo muhimu katika kusambaza nyimbo hizo kimataifa.

# Kiswahili katika Ustawi wa Vijana na Nafasi Yake katika Kudumisha Amani na Maendeleo Endelevu kwa Vijana Afrika Mashariki



**Ali Haji Hassan**

ali.hassan@zyc.go.tz

Makala hii inakusudia kufafanua nafasi ya lugha ya Kiswahili katika ustawi wa vijana na kudumisha Amani. Kwa upande wa Afrika Mashariki, vijana kuanzia umri wa 15 hadi 35 wanachukua sehemu kubwa ya wakazi, wake. Kiswahili ni nguzo ya kuleta ustawi wa vijana. Kwa mfano, kupitia elimu Kiswahili kinaweza kutumika kuwapa elimu vijana juu ya namna ya kujitambua, uzalendo na kujikwamua kimaisha. Makala hii inaonesha kuwa, kupitia vipaumbele vya maendeleo na ustawi wa vijana kama vile elimu, afya, usawa wa kijinsia, uimarishaji wa amani na usalama, teknolojia ya habari na mawasiliano, ustawi wa vijana unapatikana kupitia suala la amani na utulivu. Hivyo, kinasaidia vijana kufikia malengo endelevu ya dunia, hususani lengo Na. 16 linalosisitiza suala la amani pamoja na haki.

**Isitilahi muhimu:** Diplomasia, ustawi, endelevu



# Ubunifu wa Kaulimbiu za Kiswahili za Kuhamasisha Amani Nchini Tanzania





**Alpha Kavishe, Issaya Lupogo & Mustapha Almasi**

alphakavishe@gmail.com, islupogo@gmail.com & amustapha@mzumbe.ac.tz

Amani ni kitu muhimu kwa kila Taifa. Ingawa Tanzania imejijengea sifa ya kuwa nchi ya amani, hivi karibuni, vimeonekana viashiria vinavyohatarisha amani. Kundi linalohusika na viashiria hivyo kwa kiasi kikubwa ni vijana. Makala hii inatambulisha kaulimbiu mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili za kudumisha amani na kupendekeza njia muafaka za kusambaza kaulimbiu hizo. Mbinu ya kukusanya data iliyotumika ni mahojiano na majadiliano. Nadharia ya IsimuJamii, kupitia msingi wake wa kuchunguza uhusiano wa lugha na jamii husika, ilitumika. Makala inaibua kaumbiu 25 za amani kwa lugha ya Kiswahili, zikiwamo: *kuchezea amani ni kuchezea utu wako*, *amani ni utajiri na si umasikini*, *amani kwanza vurugu isubiri*, na *amani moyoni ni tulizo akilini*. Makala inapendekeza kuwa njia ya kusambaza kaulimbiu ni kuzifanya zitumike au zisomwe na vijana, hususan katika shule za msingi na sekondari.

**Istilahi za Msingi:** Amani, kaulimbiu za kiswahili, ubunifu

# Tafsiri katika Kiswahili na Mabadiliko ya Uchumi wa Kidijiti



**Amour Salim Said**

amour.said2017@gmail.com

Makala hii inachambua namna Kiswahili, kupitia tafsiri katika mabadiliko ya sasa ya ulimwengu, kinavyoweza kuchangia katika kuimarisha na kukuza uchumi wa kidunia. Kutokana na kasi ya mabadiliko ya ulimwengu. Tafsiri kupitia lugha mbalimbali zimekuwa jambo muhimu katika maendeleo ya uchumi wa ulimwengu. Kihistoria, tafsiri imekuwa na mabadiliko, faida na tija mbalimbali katika ngazi tofauti. Mabadiliko katika tafsiri na maendeleo yake katika kukuza uchumi wa kidunia yanahitajika kuelezwa waziwazi, kufanyiwa uchambuzi wa kina namna yanavyoweza kukuza uchumi wa kiulimwengu katika zama za sayansi na teknolojia na katika utamaduni wa mawasiliano mapana ya kikanda na kimataifa. Katika ulimwengu wenye mabadiliko ya kudumu na ya papo kwa papo, tafsiri katika Kiswahili si suala la kiisimu pekee, bali ni daraja linalowaunganisha wanajamii wa nchi mbalimbali, tamaduni za nchi tofauti na ujuzi wa mambo mbalimbali. Utafiti huu umefanywa kupitia maandiko ya kiutafiti yanayohusiana na tafsiri na nyaraka nyengine zinazohusiana na taaluma ya tafsiri.

**Dhana Muhimu**: Mabadiliko ya ulimwengu na tafsiri katika Kiswahili

# Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza Uchumi wa Taifa la Tanzania



**Anna N. Kyamba**

annanicholausk@gmail.com

Makala haya yanakusudia kutoa mchango wa Kiswahili katika kimarisha uchumi wa taifa la Tanzania, hasa katika kipindi hiki cha utandawazi. Kiswahili kinazidi kutumika katika nyanja mbalimbali za maisha, ikiwamo majukwaa ya kibiashara ndogo na za kati. Wajasiriamali wanatumia lugha hii kufikia wateja wengi kupitia mitandao ya kijamii kama vile *WhatsApp*, *Instagram* na *Facebook*. Aidha, programu mbalimbali zinazotafsiri au kufundisha mambo mbalimbali, kama vile afya, kilimo, na elimu, kwa Kiswahili zinaibuka. Vyuo kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu Mzumbe vinaendelea kutoa walimu na wataalamu wa Kiswahili wanaotumika ndani na nje ya bara la Afrika. Hii ni fursa ya kiuchumi kwa kuwa Kiswahili kinatumika kama bidhaa, ambapo wageni mbalimbali wanakuja kujifunza Kiswahili. Kadhalika, Kiswahili kina mchango mkubwa katika kuonyesha, kuhamasisha, kutangaza, kuelezea vivutio mbalimbali yanavyochangia kukuza uchumi wa taifa.

**Maneno ya Msingi**: Kiswahili, Uchumi na Taifa la Tanzania.

# Sera ya lugha nchini Burundi na athari zake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili



**Bamporubusa Mathieu**

bamat_nven27@yahoo.fr

Makala hii inatathmini sera ya lugha nchini Burundi na kuweka hadharani athari zake katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Makala inatumia Nadharia ya Mpango wa Lugha. Utafiti uliozaa makala hii ulitumia mbinu ya uchunguzi wa maandishi rasmi. Matokeo yalionesha kuwa, kutothaminiwa kwa Kiswahili na sera ya lugha nchini Burundi kulikididimiza maana Warundi wengi wanakidharau ikilinganishwa na lugha nyingine za kigeni zilizo rasmi, shuleni Kiswahili kinafundishwa kwa saa chache ikilinganishwa na Kifaransa na Kiingereza. Kiswahili hakina walimu wenye elimu ya kutosha, uhaba wa zana za kufundishia ulidhihirika pia. Makala inapendekeza upangaji madhubuti wa lugha na sera ya elimu-jumuishi, kuipa Kiswahili hadhi ya lugha rasmi na kuitumia katika mikutano ya kikazi na rasmi kama ilivyo katika nchi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki; kujenga makubaliano na Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kenya ili kupeana walimu na kurahisisha mbinu ya Kuishi na Familia Wenyeji kwa wanafunzi hasa wa vyuo vikuu vya Burundi kwa ajili ya maendeleo ya Kiswahili.

**Maneno muhimu**: Sera ya Lugha, Kiswahili, Ufundishaji na Ujifunzaji, Burundi.

# Kiswahili na Utangamano wa Kimataifa

**Chifu Said Mohamed Said (Chifu Kapere)**

**mwenekapufi@gmail.com**

Makala hii inalenga kuchambua mchango wa Kiswahili kama chombo cha kuimarisha uhusiano wa kimataifa, kukuza diplomasia ya uchumi, na kuleta mshikamano wa kijamii miongoni mwa mataifa. Kiswahili, kama lugha inayozungumzwa na zaidi ya watu milioni 200 barani Afrika na kutambuliwa na Umoja wa Afrika kama mojawapo ya lugha rasmi, kinaendelea kuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano, biashara, na ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Lugha hii imevuka mipaka ya Afrika Mashariki na kuwa daraja la kuunganisha tamaduni, kuimarisha amani, na kuwezesha majadiliano ya kiuchumi katika nyanja za biashara, uwekezaji, utalii, na ubunifu wa kiutamaduni. Makala hii inalenga kujadili namna Kiswahili kinavyoweza kutumika katika diplomasia laini, kukuza utambulisho wa Kiafrika, na kuongeza ushiriki wa Afrika katika uchumi wa dunia. Aidha, inatoa mapendekezo ya namna ya kuendeleza Kiswahili kama nyenzo ya kimkakati katika sera za nje, majukwaa ya kimataifa, na taasisi za kielimu ili kuimarisha amani, mshikamano na ustawi wa pamoja.

# Onomastiki ya Ulem avu katika Methali za Waswahili: Elimu kwa Mtazamo wa Maarifa Asili



**Wanjala C. N. Simiyu**

wsimiyu@kibu.ac.ke

Kiswahili kama lugha ya Kiafrika inabeba maarifa muhimu yanayoweza kutumiwa kustawisha juhudi za kidiplomasia na amani miongoni mwa jamii mbalimbali. Maarifa haya yanawasilishwa kupitia fasihi, hasa utanzu wa methali. Methali hizi hundwa kutokana na maneno yaliyoteuliwa kwa maksudi kabisa ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Taaluma ya Onomastiki inahusika na hali ya kuvipa viumbe majina kwa mujibu wa mila na desturi za jamii husika. Ulemavu ni hali ya kuwa na hitilafu au upungufu fulani mwilini au akilini inayomzuia mtu kutekeleza shughuli za kawaida. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu methali na suala la ulemavu bila kuhusisha na suala la Kiswahili na elimu kuhusu maadili ya kijamii. Kwa hivyo basi, makala hii inanuia kuchambua methali za Kiswahili kwa jicho la maarifa asili ili kuibua kitovu cha maana fiche katika methali zinazotumia onomastiki za ulemavu. Methali husika zitachambuliwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uwazimu ya Hegel. Makala hii inadhamiria kuonesha kwamba sisi wote ni walemavu ingawa hatuna ulemavu wa kuonekana na kwamba huenda huu ulemavu

usiodhirika ndio hatari zaidi katika kuifanya jamii kukosa kuzingatia elimu inayobebwa na methali hizi.

**Maneno muhimu**: Onomastiki, Ulemavu, Uwazimu, Unyanyapaa.

# Mbinu za Uhunthishaji wa Wahusika katika Filamu za Kiswahili: Mifano kutoka Vichekesho vya Joti na Dulvani.



**Diana Remias**

dianaremias21@gmail.com

Makala hii inachambua mbinu za uhunthishaji wa wahusika katika filamu za vichekesho za Kiswahili nchini Tanzania. Data hizo zilikusanywa kutoka mtandao wa *Tiktok* na *Instagram*. Aidha, zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa vilongo pamoja na usimbishaji wa maudhui. Utafiti uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Uwakilishi. Mbinu za uhunthishaji zilizobainika kutumiwa na wahusika wa filamu za vichekesho ni: kubadili sauti kuwa ya kike, kutembea mwendo wa kike, kuolewa, pamoja na kubadili muonekano wa nje, yaani kujiremba, kupaka kucha rangi, kuvaa mawigi na wakati mwingine kusuka nywele mitindo ya kike, kuvaa mavazi ya kike, hasa yanayobana, kujiwekea maziwa hali kadhalika makalio. Makala inapendekeza kuwa tafiti mbalimbali zifanyike ili kubainisha zaidi sababu za uhunthishaji wa wahusika katika filamu za vichekesho za Kiswahili.

# Kiswahili na Amani

**Elizabeth Luena Lyimma**
lyimma.elizabeth@yahoo.com

Makala hii inafafanua mchango wa lugha ya Kiswahili katika ujenzi wa amani duniani kupitia nyanja kuu tatu: Diplomasia ya kitamaduni, mifumo ya elimu, na ubunifu wa kifasihi. Mbinu ya uchambuzi wa matini na mahojiano zimetumika ili kuonyesha kuwa Kiswahili si lugha ya mawasiliano tu, bali ni mfumo wa thamani unaohubiri amani. Matokeo yanabainisha kuwa upanuzi wa Kiswahili nchini Ufaransa na barani Ulaya unatoa fursa mpya za ushirikiano ya kiusalama na kimaendeleo. Makala inahitimisha kwa kutoa mapendekezo ya kisera ya jinsi ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili katika majukwaa ya kimataifa ili kufikia malengo ya amani endelevu na maendeleo ya pamoja.

**Dhana za Msingi**: Kiswahili, Diplomasia ya Kitamaduni, Rais Samia Suluhu Hassan, Fasihi ya Amani, Elimu Jumuishi.

# Matumizi ya Akiliunde kama Nyenzo ya Tafsiri katika Ujifunzaji wa Kiswahili: Uzoefu Kutoka Chuo Kikuu cha Ghana



**Hadija Jilala**

dijaah@yahoo.com au hadija.jilala@out.ac.tz

Makala hii inahusu matumizi ya Akiliunde kama nyenzo ya tafsiri katika ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia uzoefu wa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili nchini Ghana. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili na dodoso. Makala inasisitiza kuwa Akiliunde, kama nyenzo ya tafsiri, inaweza kumsaidia mjifunzaji wa lugha kujifunza lugha. Pia, inaweza kupotosha uteuzi wa misamiati, visawe vya maneno na hata kuathiri maana na ujumbe uliokusudiwa. Hivyo, makala inapendekeza kuwapo kwa umakini katika matumizi ya akili ya mwanadamu katika kuchakata zao lililotokana na akiliunde.

# Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza Uchumi Baina Tanzania na Comoro



**Ibrahima Mohamed Ibrahim**
poeteibrahima@gmail.com

Maendeleo ya Kiswahili yanatoa mwanga wa matumaini kwa maendeleo ya kiuchumi ndani na nje ya Afrika Mashariki kwa kuwa mawasiliano ya wakazi wake yanarahisisshwa kwa kutumia lugha hii ya mawasiliano mapana. Hatua hii tayari ilitangaza kufunguka kwa wakazi hao kwa kuwa Kiswahili kimekuwa lugha ya uchumi katika nchi kadhaa. Kwa mfano, wakati wa ziara rasmi nchini Comoro mwaka 2025, Rais wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, alitangaza kuwa Comoro inachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa Tanzania. Akaeleza nia yake ya kuona kuwa lugha ya Kiswahili ikifundishwa nchini Comoro ili kuimarisha ushirikiano huu wa kiuchumi wa nchi hizi mbili kupitia shughuli mbalimbali za kiuchumi na kiutamduni. Ni dhahiri kwamba lugha hii ikitumiwa vema inaweza kuchochea fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na utalii, biashara na ushirikiano wa kijamii. Hivyo, makala hii inalenga kuangazia fursa zilizopo na namna ya kuzichangamkia kwa manufaa ya jamii zote na lugha yenyewe.

# Nguvu ya Kiswahili Katika Diplomasia ya Kitamaduni na Maendeleo ya Utalii



**Lorna B. Mwijarubi**

anrolbonny@gmail.com

Lengo la makala hii ni kuchambua nguvu ya Kiswahili kama nyenzo ya diplomasia laini inayochangia kukuza uelewa wa utamaduni, mshikamano wa kimataifa, na maendeleo ya utalii endelevu. Utafiti ulitumia mkabala wa kimaelezo kupitia mapitio ya nyaraka mbalimbali. Kwa kuzingatia maono ya UNESCO kuhusu kulinda urithi wa utamaduni usiogusika, makala hii inabainisha jinsi Kiswahili kinavyotumika kama daraja la mafanikio la kuunganisha utamaduni na utalii, inaeleza namna matumizi ya Kiswahili katika sekta ya utalii yanavyoongeza thamani ya lugha ya Kiswahili kwa watalii, kuimarisha ushiriki wa jamii za wenyeji, na kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kupitia mtazamo wa diplomasia ya elimu, nafasi ya Kiswahili ni kubwa katika kuimarisha ushirikiano wa kitaaluma, tafiti, na mafunzo kati ya taasisi za Ufaransa na Afrika. Makala hii inahitimisha kuwa Kiswahili ni rasilimali ya kimkakati na moja ya tunu za taifa letu na maendeleo endelevu ya utalii.

**Maneno Muhimu:** Kiswahili, Diplomasia ya kiutamaduni, Maendeleo ya utalii, Ufaransa- Afrika.

# Dhima ya Lugha katika Kuibua Wanadiplomasia Bobevu: Uchunguzi katika Ufundishaji Kiswahili katika Ngazi ya Elimumsingi



**Maryam Y. Mwinyi**
mayumwi@gmail.com

Makala hii inafafanua dhima ya lugha katika kuibua wanadiplomasia bobevu, huku ikiangazia ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika ngazi ya elimumsingi. Data zilipatikana uwandani na maktabani. Makala hii inaongozwa na nadharia ya mtaji wa lugha yenye msingi mkuu kwamba lugha ni rasilimali muhimu ya kijamii inayoweza kumpa mtu nguvu, hadhi na fursa katika jamii. Ni wazi kuwa bila ya kumudu lugha ipasavyo tangu ngazi ya elimumsingi, ufanisi katika diplomasia hauwezi kupatikana. Hivyo basi, elimumsingi ni chimbuko la wanadiplomasia bobevu kwa kuwa hapo ndipo umahiri wa lugha hujengwa na kukomazwa. Kwa sasa, elimumsingi hutolewa kwa miaka kumi kwa watoto wa umri wa miaka 4 hadi 15, umri ambao ni sawa na shamba lenye rutuba ambamo mbegu ya lugha na maadili ikipandwa vyema huzaa mawasiliano madhubuti na yenye tija kitaifa na kimataifa. Kwa muktadha huo, uimara wa lugha katika diplomasia unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha husika katika elimumsingi.

# Nafasi ya Kiswahili katika Utangamano wa Kimataifa kwa jicho la Ubuntu

**Meinrad Haule Lembuka**

meinradlembuka@gmail.com

Andiko hili limetumia nadharia ya Ubuntu katika kupitia nafasi ya lugha ya Kiswahili katika utangamano wa Kimataifa. Matokeo yanaonyesha kuwa kushabihiana kwa Ubuntu na Kiswahili hakujapewa nafasi na utafiti unaostahili katika utangamano wa Kimataifa kwa sababu ya masalia ya muktadha wa kikoloni katika mifumo ya Kiafrika ikiwemo elimu. Taarifa na uzoefu zinaonyesha kuwa Kiswahili kina nafasi ya kipekee kama kiunganishi kikuu cha utangamano wa kimataifa, kikiendeleza utamaduni wa Ubuntu wa "utu", umoja, na ushirikiano. Julai 2021, UNESCO iliiweka rasmi tarehe 07 Julai kuwa ni siku ya Kiswahili Duniani na 2025 ilitangazwa kuwa lugha rasmi ya UNESCO. Hivyo basi, ushabihiano wa Kiswahili na Ubuntu unapelekea kuifanya kuwa lugha ya umoja na udugu kama falsafa ya Ubuntu inavyosisitiza kuleta umoja, ushirikiano, uhuru, maelewano, na ujamaa kwa lengo la kukuza utangamano wa kikanda na kimataifa.

# Nafasi ya Kiswahili katika kujenga utangamano wa kimataifa nchini Uganda



**Monday Geofrey Akol Amazima**

mwalimakol@gmail.com

Lengo la makala hii ni kujadili nafasi ya Kiswahili katika kujenga utangamano wa kimataifa nchini Uganda. Uganda imekuwa sehemu ya maendeleo endelevu ya Kiswahili licha ya kwamba kumekuwa na baadhi ya viongozi na jamii ambao wamekuwa wakipinga vikali matumizi ya Kiswahili. Kupitia wanaharakati na tasnia mbalimbali kama elimu, vyombo vya usalama, vyombo vya habari, sanaa, michezo na tekinolojia, Uganda imetoa mchango si haba katika matumizi ya Kiswahili ili kujenga utangamano wa kimataifa. Kwa kuridhia mikataba na itifaki mbalimbali zinazotambua Kiswahili kama lugha ya mawasiliano mapana ya kikanda, Uganda imekuwa miongoni mwa nchi ambazo zinakienzi Kiswahili. Makala inaongozwa na nadharia ya kuweka ajenda kwa kuangazia nafasi ya Uganda katika matumizi ya Kiswahili ili kujenga utangamano wa kimataifa. Viongozi, kama vile Hayati Iddi Amin na Rais wa sasa, Mhe. Yoweri Museveni, wametumia ushawishi wao kama wanaujumuiya wa Afrika kukipa hadhi Kiswahili kisheria na kimazoea. Tangu Kiswahili kitangazwe kuwa na siku yake ya Kimataifa Duniani, kimeendelea kutumiwa kuimarisha amani, mshikamano na diplomasia ya uchumi duniani ikiwa ni pamoja na nchini Uganda.



# Dhima ya Kiswahili katika Kujenga Utambulisho wa Kitaifa Kupitia Mfumo wa Elimu



**Saade Said Mbarouk, Mwanahija Ali Juma na Asha L. Ibrahim**

mwanahijajuma1@gmail.com

Makala hii inajadili dhima ya lugha ya Kiswahili katika kujenga na kuimarisha utambulisho wa kitaifa kupitia mfumo wa elimu nchini Tanzania. Utambulisho wa kitaifa hujengwa kupitia mfumo wa elimu, lugha sanifu na taasisi za dola zinazowaunganisha watu chini ya utamaduni mmoja. Aidha, dola huchagua lugha rasmi na kuisambaza kupitia elimu na utawala; hatimaye hutokea utambulisho wa kitaifa kwa sababu watu huwa katika mfumo mmoja wa utamaduni. Lugha pia ni mhimili wa mawasiliano, ni chombo cha kuunda fikra, maadili na mshikamano wa kijamii. Kupitia nadharia ya utaifa na nadharia ya lugha kama chombo cha utambulisho, makala hii inabainisha namna Kiswahili kilivyotumika kama nyenzo ya kuunganisha makabila mbalimbali na kujenga hisia ya umoja wa kitaifa. Data za utafiti uliozaa makala hii zimepatikana maktabani. Matokeo yanaonesha kuwa mfumo wa elimu umekuwa mhimili mkuu katika kusambaza Kiswahili kama lugha ya pamoja, hivyo kuimarisha utambulisho wa taifa. Hata

hivyo, kuna changamoto katika sera ya utamaduni na ya elimu ambamo masuala ya lugha hutajwa. Pia, kuna changamoto katika utandawazi. Makala inapendekeza kuimarishwa kwa matumizi ya Kiswahili katika ngazi zote za elimu ili kulinda utambulisho wa kitaifa.

# Nafasi ya Akiliunde katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni katika Mkabala wa Kimawasiliano



**Nasra Habibu & Salma Hamad**

nasramtani@gmail.com

Lengo la makala hii ni kubainisha mchango wa Akiliunde katika kuendeleza na kuimarisha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji lugha katika mkabala wa Kimawasiliano ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji Kiswahili kama lugha ya kigeni. Akiliunde ni taaluma ya sayansi ya kompyuta inayojihusisha na kutengeneza mifumo au programu zinazoweza kufanya kazi zinazohitaji maarifa ya kibinadamu. Akiliunde imetokana na kasi ya maendeleo ya kiteknolojia ulimwenguni, ambapo ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za kigeni umechukua sura mpya. Matumizi ya TEHAMA yamekuwa nyenzo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji lugha za kigeni. Kuna tafiti chache ambazo zimeshughulikia namna Akiliunde inavyoweza kutumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni. Mbinu ya usaili imetumika kukusanya taarifa muhimu za utafiti uliozaa makala hii. Matokeo yanaonesha kuwa Akiliunde ina mchango mkubwa katika kuimarisha mbinu za kimawasiliano mbali na kuwepo changamoto kadhaa.

**Maneno muhimu:** Akiliunde, mbinu za kimawasiliano, Kiswahili, lugha ya kigeni.



# Kiswahili: Msingi wa Uhuru wa Kidijitali kwa Vijana

**Onesmo S. Nyinondi**

onesmoni@gmail.com

Makala hii inajadili mfumo wa sera wa Uhuru wa Kidijiti wa Lugha kwa Vijana wa Afrika kwa kutumia Kiswahili kama lugha ya kimkakati, kwa kuangazia: (i) Kiswahili kama miundombinu ya AU na haki ya vijana katika uchumi wa data; na (ii) fursa za ajira kupitia teknolojia za lugha. Katika enzi ya Akiliunde na uchumi wa data, lugha zimegeuka kuwa miundombinu ya kimkakati ya maarifa, nguvu ya kidiplomasia, na msingi wa ujumuishi wa kijamii na kiuchumi. Licha ya Kiswahili kutambuliwa kimataifa, bado kinawakilishwa kwa kiwango kidogo katika miundombinu ya AU, korpasi za data na teknolojia za lugha. Hali hii inatishia ujumuishi wa vijana katika uchumi wa kidijiti unaoendeshwa na data. Jitihada za kimataifa kama Masakhane pamoja na taasisi kama ACTS, Kituo cha Sayansi ya Data kwa Athari za Kijamii, na Taasisi ya Afrika ya Sayansi ya Data na Akiliunde, zimeanza kujenga data na zana za lugha za Kiafrika, zikionesha mwelekeo mpya wa umiliki wa maarifa na teknolojia katika nchi zinazoendelea. Makala inapendekeza sera za uwekezaji katika korpasi za Kiswahili, ujumuishaji wa lugha katika sera za AU na uwezeshaji wa vijana wabunifu wa teknolojia za lugha.

# Kusimamia Haki ya Kijamii Darasani: Uchunguzi wa Mbinu za Ukuzaji wa Kiswahili katika Mazingira ya Kielimu Yenye Lugha Nyingi

**Said S. Khassim**

saidisudijk@gmail.com

Wasilisho hili litaangazia jinsi Kiswahili kinavyoweza kutumiwa kama nyenzo ya kijamii na kielimu katika darasa lenye lugha nyingi, hasa likilenga kukuza uhusiano na uelewa wa wanafunzi. Kwa kutumia mbinu ya utafiti wa kesi binafsi, tuliangalia utekelezaji wa mikakati ya lugha mseto, ikihusisha Kiswahili na Kiingereza, katika darasa la chekechea nchini Tanzania. Kupitia uchambuzi wa mwingiliano darasani, mahojiano na mawasilisho ya wanafunzi kwa kutumia mbinu za kisayansi, matokeo yanaonesha kuwa kuruhusu na kutumia Kiswahili kimasomo kuliongeza ushiriki wa wanafunzi, kuliboresha uelewa wa dhana ngumu, na kukuza mazingira ya kujumuika. Ingawa baadhi ya walimu wanaweza kuwa na wasiwasi kuhusu maendeleo ya Kiingereza kwa wanafunzi, utafiti uligundua kuwa Kiswahili kilitumika kama daraja la kufikia umahiri wa lugha ya kufundishia. Hivyo, lugha ya Kiswahili ikipewa thamani kama lugha ya kufundishia katika mazingira ya kielimu yenye lugha nyingi, itachagiza msingi wa haki ya kijamii katika elimu ya kitaifa na kimataifa na kukuza uchumi.



# Mchango wa Akiliunde katika Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kwenye Diplomasia ya Kidijiti na Uchumi wa Dunia

**Shaban Rashid Said**

kisleufahari@gmail.com

Katika ulimwengu unaozidi kutegemea mifumo ya kidijiti, lugha ya Kiswahili inakabiliwa na fursa na changamoto katika kuhakikisha inapata nafasi stahiki kwenye majukwaa ya kimataifa. Lengo kuu la makala hii ni kuchambua namna zana za Akiliunde, kama vile mifumo ya tafsiri ya papo hapo na uchakataji wa lugha asilia zinavyoweza kutumika kuvunja vizuizi vya mawasiliano katika biashara na uhusiano wa kimataifa. Aidha, makala hii inajadili umuhimu wa kuingiza data sahihi za Kiswahili sanifu kwenye mifumo ya Akiliunde ili kuepuka upotoshaji wa kimaana ambao unaweza kuathiri makubaliano ya kidiplomasia. Vilevile, makala hii inaangazia nafasi ya vijana wabunifu wa teknolojia nchini Tanzania na Afrika Mashariki katika kutengeneza kanzidata zinazozingatia utamaduni na misingi ya Kiswahili. Hitimisho la makala litatoa mapendekezo ya kisera kwa mamlaka husika na wadau wa teknolojia kuhusu namna ya kutumia akiliunde kama daraja la kukiimarisha Kiswahili kuwa lugha ya kibiashara na kidiplomasia duniani, sanjari na malengo ya Kongamano.



# Urazini wa Diplomasia ya Uchumi katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya Makuwadi wa Soko Huria

**Stela Faustine**

stella.faustine@udom.ac.tz

Makala hii inachambua namna diplomasia ya uchumi inavyoyanufaisha mataifa washirika pamoja na changamoto zinazojitokeza kama inavyosawiriwa katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria*. Uchambuzi wa matini umeongozwa na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Matokeo yanaonesha kuwa uhusiano wa kidiplomasia katika muktadha wa kiuchumi umeendelea kuyapa manufaa makubwa mataifa ya Magharibi kuliko yale ya ulimwengu wa tatu. Hali hii inachangiwa na ukweli kwamba mikataba ya kifedha, uwekezaji wa kigeni na upatikanaji wa masoko inatekelezwa kwa namna inayoyawezesha zaidi mataifa yaliyoendelea kunufaika kiuchumi. Mataifa yanayoendelea yamebaki katika nafasi duni ya kiushindani na kunufaika kwa kiwango kidogo, huku yakikabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile upungufu wa mitaji, vikwazo vya kibiashara, na ukosefu wa masoko. Kwa jumla, ili diplomasia ya uchumi iwe na manufaa sawa kwa pande zote, inapendekezwa kuundwa kwa sera jumuishi za kiuchumi zitakazosaidia kuleta mzani sawia miongoni mwa mataifa washirika na kutumia uga wa fasihi kuhamasisha diplomasia ya haki.



# Urazini wa Diplomasia ya Uchumi katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya Makuwadi wa Soko Huria

**Theresia Bonface Mbogo**

theresia.mbogo@out.ac.tz

Kiswahili ni lugha ya taifa na kimataifa inayochangia kwa kiasi kikubwa katika mawasiliano, utambulisho wa kitamaduni na utoaji wa huduma katika sekta ya utalii. Ingawa lugha ya Kiingereza hutumika zaidi katika utalii wa kimataifa, lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika pia. Maeneo ambayo Kiswahili hutumiwa kuboresha ubora wa huduma, kukuza mwingiliano wa kitamaduni na kuongeza uzoefu wa wageni bado hayajachunguzwa kwa kina. Makala hii inabainisha maeneo mbalimbali ambamo wahudumu wa hoteli na watalii kutoka Ufaransa wanavyowasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Mbinu za usaili, ushuhudiaji na usomaji matini zilitumika kukusanya data. Data zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Kimaeneo (NUK). Matokeo yanaonesha kuwa maeneo ambamo lugha ya Kiswahili hutumika ni mapokezi, eneo la kulia chakula, eneo la nje ya hoteli, na kwenye maandishi ya mabango na matangazo. Aidha, upanuzi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika huduma za utalii unaongeza thamani ya sekta ya utalii na kuinua utalii wa kitamaduni. Makala hii ambayo inachangia katika taaluma za isimu-jamii na usimamizi wa utalii,

inapendekeza kuandaa programu maalum za mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa watalii kutoka Ufaransa pamoja na kuwajengea uwezo wahudumu wa hoteli katika mbinu za mawasiliano ya lugha nyingi, hususan kwa wageni wanaotumia Kifaransa. Aidha, inapendekezwa kuwapo kwa juhudi za kimakusudi za kuingiza Kiswahili katika sera ya utalii na mitaala ya mafunzo ya huduma za utalii, ili kuboresha uzoefu wa watalii na kukuza hadhi ya Kiswahili kimataifa.



# Matumizi ya Fasihi ya Kiswahili katika Diplomasia ya Umma na Maendeleo ya Uchumi Endelevu

**Neema Julius Luhwago**
Neema.luhwago@udom.ac.tz

Katika enzi ya utandawazi, diplomasia ya umma imeibuka kama mkakati muhimu wa mataifa kujenga taswira chanya, kukuza maelewano ya kimataifa na kuvutia ushirikiano wa kiuchumi. Tanzania, kama taifa linalotumia Kiswahili kama lugha ya taifa na kimataifa, ina hazina kubwa ya fasihi ya Kiswahili inayojumuisha fasihi simulizi, riwaya, tamthilia na ushairi. Fasihi hii imekuwa chombo muhimu cha kuwasilisha historia, maadili, utamaduni na falsafa ya jamii ya Watanzania kwa hadhira ya ndani na ya kimataifa. Hata hivyo, mchango mahsusi wa fasihi ya Kiswahili katika diplomasia ya umma na maendeleo ya uchumi endelevu bado haujaangaliwa kwa kina katika tafiti nyingi za kitaaluma. Hali hii inazua haja ya kufafanua jinsi fasihi ya Kiswahili inavyoweza kutumika kimkakati katika kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia na kuchochea maendeleo ya uchumi wa taifa. Makala hii ni ya kitaamuli, ikiongozwa na Nadharia ya Diplomasia ya Umma. Data za utafiti wa makala zilipatikana kwa njia ya uchambuzi matini na usaili. Makala inafafanua kuwa fasihi ya Kiswahili huchangia kuimarisha diplomasia kupitia maudhui yanayosisitiza amani, mshikamano na utambulisho wa kitaifa, hali inayochochea fursa za uchumi endelevu kama vile utalii wa kitamaduni, uchumi wa ubunifu na ajira katika sekta za sanaa na

utamaduni. Makala inapendekeza kuwa matumizi ya kimkakati ya fasihi ya Kiswahili katika diplomasia ya umma ni nyenzo muhimu katika kuimarisha mahusiano ya kimataifa na kuchochea maendeleo ya uchumi endelevu nchiniTanzania.

Maneno Muhimu: Fasihi ya Kiswahili, Diplomasia ya umma, Uchumi endelevu



# Kwa nini ni Lazima Kuenzi Utamaduni Wetu?

**Omar Salum Mohamed**
Omaaar23@yahoo.com /
omar.mohamed@utamaduni.go.tz

Duniani kote, watu huishi kwa namna ya utamaduni wao unavyoelekeza. Nyanja zote za maisha ya mwanadamu huongozwa na utamaduni wake. Kwa upande wa Nchi ya Tanzania, utamaduni wake huiongoza jamii wajibu wake wa kutunza na kulinda amani, utulivu, upendo, huruma, imani, umoja, ukarimu na utu. Tunu hizi ambazo hudhihirika kupitia tabia, mienendo na matendo siyo tu zinatujengea heshima bora, bali pia huwa vivutio kwa wageni kutoka mataifa mbalimbali. Kwa kutambua hilo, nchi ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuanzisha vituo vya Kiswahili na utamaduni kwa jumla kupitia balozi zake zilizo katika nchi mbalimbali. Jambo hili linapofanyika na kuendelea huwa njia mojawapo muhimu katika kukisambaza Kiswahili ulimwenguni na utamaduni wake. Hivyo, ikiwa Serikali zetu zinachukua jitihada kubwa za namna hiyo, ni vema wananchi nao wakaunga mkono ili kuhakikisha utamaduni wake unaendelea kutunzika, kuimarika, kuhifadhika na kuendelea kurithiwa na kila kizazi baada ya kizazi. Hivyo, makala hii inalenga kujadili njia za kuenzi utamaduni na kuueneza kila taifa ili hatimaye uweze kuwa kigezo chema kwa tamaduni nyengine.

# Kwa nini ni Lazima Kuenzi Utamaduni Wetu?



**Sarah Vincent**

sarahvicent@yahoo.com

Makala hii inafafanua Nafasi ya Kiswahili katika Kuhamasisha Diplomasia na Maendeleo ya Uchumi Duniani kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yanayoendelea katika mfumo wa utandawazi. Kiswahili, kama lugha inayozungumzwa na mamilioni ya watu ndani na nje ya Afrika, kimeendelea kupata hadhi ya kimataifa kupitia matumizi yake katika taasisi za kikanda na kimataifa, zikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU) na mashirika ya kimataifa kama UNESCO. Hivyo, ilikuwa muhimu utafiti huu kufanyika ili kuonesha matumizi hayo ya Kiswahili katika kuhamasisha suala la diplomasia na maendeleo ya uchumi duniani. Utafiti wa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Diplomasia ya Lugha na Nadharia ya Mtaji wa Lugha. Data za utafiti zilipatikana kwa njia ya mahojiano na uchambuzi matini na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Kiswahili huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha diplomasia ya kitamaduni, kuongeza ufanisi wa mawasiliano ya kimataifa, na kufungua fursa za kiuchumi kupitia biashara, elimu, utalii, vyombo vya habari na teknolojia za kidijiti. Aidha, matumizi ya Kiswahili katika majukwaa ya kimataifa yanaimarisha

mshikamano wa kikanda na kuongeza ushawishi wa nchi zinazokitumia katika maamuzi ya kimataifa. Utafiti huu unapendekeza kuwepo kwa sera thabiti za kukuza Kiswahili kimataifa, uwekezaji katika tafsiri na teknolojia za lugha, pamoja na kukipa Kiswahili nafasi zaidi katika diplomasia rasmi na uchumi wa maarifa, ili kukifanya kuwa nguzo muhimu ya maendeleo endelevu duniani.

**Maneno Muhimu**: Lugha ya Kiswahili, Diplomasia, maendeleo ya Uchumi

# Uhifadhi wa Urithi wa Kiswahili kwa Utalii Endelevu: Mfumo wa Kitaifa wa Mikusanyiko ya Kiswahili kupitia Bibliografia ya Taifa



**Mboni A. Ruzegea**
mboniruzegea@gmail.com

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (TLSB) ina wajibu wa kisheria wa kusimamia, kuendeleza, kuhifadhi na kusambaza huduma za maktaba nchini, ikiwemo kupokea na kuhifadhi machapisho kutoka kwa wachapishaji na waandishi wa ndani kwa mujibu wa sheria. Kupitia Kitengo cha Bibliografia ya Taifa, TLSB imehifadhi machapisho mbalimbali ya Kiswahili, yakiwemo vitabu, majarida, magazeti na nyaraka, yanayobeba historia ya lugha ya Kiswahili, mila, tamaduni, fasihi, maeneo ya urithi, miji mikongwe, mbuga za wanyama na maeneo mengine ya kihistoria. Lengo la wasilisho hili ni kuonesha namna Bibliografia ya Taifa na mikusanyiko ya Kiswahili inayohifadhiwa na TLSB inaweza kutumika kama nyenzo ya kuhifadhi urithi wa Kiswahili, kuongeza upatikanaji wa maarifa ya kitamaduni, na kuchochea utalii endelevu unaotokana na lugha, historia na maeneo ya urithi wa Tanzania. Machapisho haya yana mchango muhimu katika kuendeleza utalii wa urithi wa Kitanzania na utalii wa lugha ya Kiswahili kwa kuwa humwezesha msomaji, mtafiti na mtalii kuelewa historia, kumbukumbu na maana ya maeneo anayoyatembelea. Aidha, TLSB imeendelea kuongeza mwonekano wa Kiswahili kwa hadhira ya kitaifa na kimataifa kupitia uainishaji, uorodheshaji na usambazaji wa maudhui ya Kiswahili. Katika kuimarisha jukumu hili, matumizi ya TEHAMA

na Akili Unde yanaweza kusaidia kutambua, kuchanganua, kuhusianisha na kuwasilisha maudhui ya Kiswahili yanayohusiana na maeneo ya urithi. Kupitia maonesho ya kidijiti yanayounganisha “kitu cha kusoma” na “mahali pa kutembelea”, maktaba zinaweza kuwa miundombinu muhimu ya urithi wa lugha ya Kiswahili, zikihifadhi, zikitafsiri na kuwasilisha maarifa kwa njia inayoaminika. Hatua hii itachangia kuongeza mvuto wa maeneo ya urithi, matumizi ya maudhui ya ndani na ustawi wa kiuchumi kupitia utalii endelevu.

**Maneno muhimu:** Utalii endelevu, utalii wa urithi, Bibliografia ya Taifa, Akili Unde, maonesho ya kidijiti.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO